

SHAIRI: MS NA 234

Maelezo Juu ya Mshairi

Na

P. Ridhiwani

Mtunzi wa shairi hili, ambaye hakulitaja jina lake, alikuwa na makusudio ya kuitakasa nafsi yake kwa mambo kadha ambayo amesingiziwa. Ameandika ushairi huu ili kila mmoja afahamu yale ambayo walimwengu wanasingizia na papo akatoa maelezo ya kuyakanusha mambo hayo. Alifanya hofu kwamba ikiwa jambo linasemwa na watu kwa kulisikia tu bila ya kupata maelezo ya yule mwenye kulaumiwa kwa jambo hilo, matunda yake yatakayopatikana ni lawama la milele. Hivyo aliona ni ubora ajitakase kama mfano usemwao, "Samaki mkunje angali mbichi." Uthibitisho wa maelezo hayo ni yale aliyoyaandika mwenyewe katika ubeti wa pili na wa tatu yasemayo:

2. Wala mimi sikutaka mambo haya kutamka
Lakini nasononeka kwa niliyoyasikia.
3. Nami singeliyanena ila ninayo maana
Nacha (naogopa) yasizuke tena haya niliyosikia

Mshairi alikuwa na rafiki yake ambaye alimletea habari alizozisikia ambazo zilikuwa za uwongo, naye aka-kusudia azieleze waziwazi ili aukomeshe ubaya uliozuka.

Kwanza alitangaziwa kwamba anadaiwa naye ashindwa kulilipa deni adaiwalo. Hakubali kwamba anadaiwa kwa sababu yeye ni mtu muaminifu. Hata kama anadaiwa hawezikabisu kumkimbia mdeni isipokuwa atamfuata mdeni ampe tumaini zuri la kumlipa pindi apatapo.

Jambo la pili ambalo lilienea kusemwa katika mtaa wa Makadara mjini Mombasa ni kwamba nyumba anayokaa anadaiwa sana, hana uwezo wa kulipa na madeni adaiwayo yanam-

shinda kuyalipa. Vile vile imesemwa kwamba hiyo nyumba anayoishi huko Makadara kodi yake analipiwa. Yeye anakanusha usemi huo kwa kusema,

10. Nalipa ya chumba changu na chumba cha ndugu yangu.

Hivi leo walimwengu wanena wanilipia.

Jambo la tatu ambalo lilimfanya atangazwe ni chakula, yeye alikuwa na tabia ya kununua chakula kwa jumla aki-shirikiana na mwenziwe. Hata hivyo alitiwa dosari kwamba alacho ni kile cha mwenziwe na yeye hatowi kitu. Yeye ali-jibu kwa kusema kwamba maneno hayo ni uwongo mtupu ambao wanamzulia.

13. Mimi kwangu nala changu na mke na ndugu yangu Na atwaacho mwenzangu ni chake ajilipia.

14. Mimi kwangu sili kwake wala sinywi maji yake Nala changu ala chake silipiwi hata moyo.

Kisha akaendelea kusema kwamba iwapo maneno haya asemayo mwenzake anayakataa, basi na aje waonane uso kwa uso ili wayanene maneno hayo vizuri.

Tena akaendelea,

16. Mimi sipendi maneno yasiyo masikizano Leo huwaje hayano mwenzangu kunizulia

17. Lakini hapana kitu kwa waja ni ada yetu Yule atendae utu kwake hulipwa mabaya.

Mpaka hapa mshairi aligota kuelezea yale mambo ambayo yalitangazwa na watu bila ya kuwa na uhakika wake. Halafu aliendelea kuliezeza hili jambo la shirika ya chakula akasema, "Mimi yasingenifika yote haya isipokuwa ni mke wangu Aswila ndiye aliyetaka. Mimi sikupenda kula na mtu shirika kwa sababu nilifahamu matatizo yake. Tangu sasa sitaki tena kushirikiana na mtu kwa kuogopa isije ikanifikasi balaa. Mimi sikutaka asilani kula chakula shirika lakini mwenzangu ndiye aliyenitaka nami nikaona ni afadhali nimkubalie. Kama ningeyajua mwanzo kama mambo yatakuwa hivi, ningejitenja mapema ili isinifike balaa.

"Tangu sasa nitajitoa katika shirika; nitapika chakula changu peke yangu. Wakati nitakapopika chakula

changu sitavunja kawaida yangu ya kupeana baina yangu na mwenzangu. Mimi nikipika nitampa na yeye akinipa chake nitakipokea. Siwezi kumkasirikia kwa yote ambayo amenitenda na iwapo atahama hakuna lolote ambalo kwangu litapungua. Sitazungumza lolote katika yale ambayo nimemtenda kwani Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyafahamu yote, lakini pindi utokeapo mjadala wa kukusanyika watu wakati huo niko tayari kusema jambo moja baada ya moja. Wakati huo sitanyamaza kwa kufichaficha mambo, kwani sipendi kusengenyana na kuficha mambo. Mimi ni mtu nipendae mwendo ulio sawasawa.

Beti zake za mwisho katika kujitakasa zasema:

31. Wala sichi kutamka kwa jambo lenye hakika
Muungwana hufunuka hafiti lilolekea
32. Na mwenye kucha kunena akawa husengenyana
Huyu hawi na maana ni muovu wa dunia
33. Na wala hawi ni mtu mwenye kusifia watu
Huitwa ni nyoka chatu aumaye kivivia
34. Nami naomba wendani alo na neno moyoni
Nanikabili matoni nasiniche kunambia
35. Na hapa nilipokoma ndio mwisho wa kalima
Rabi tanipa salama ya akhera na dunia.

MAELEZO YA MHARIRI

Huu ni utenzi mzuri sana ambao umepatikana katika miswada iliyoandikwa kwa hati ya Kiarabu ambayo imehifadhiwa katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hajulikani mtunzi ni nani na aliishi lini, japo yaelekeea aliishi Mombasa. Msomaji yejote ambaye ana taarifa zaidi juu ya mtunzi wa utenzi huu tunaomba atuandikie kwenye anwani ifuatayo: Mhariri, Kiswahili, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania.